
# Zab. 137 - Ni Mtakatifu

## Siku ya Mungu ya tano katika Mwaka C

M: Jeannot Amani Mulume




## Shairi: 1-2a, 2bc-3, 4-5, 7c-8

1. Nitakutukuza,ee Bwana, kwa moyo wangu **wote**,
   kwani umesikia maneno ya kinywa **changu**.
   Mbele ya malaika nitakui**mbi**a,
   nitaliangukia hekalu lako taka**tifu**.

2. Nitatukuza jina **lako**,
   kwa ajili ya wema na uaminifu **wako**.
   Siku nilipokuita ulinisiki**li**za,
   uliongeza nguvu rohoni **mwangu**.

3. Wafalme wote wa dunia watakutukuza, ee **Bwana**,
   watakapo sikia maneno ya kinywa **chako**.
   Wataziimbia njia za **Bwa**na:
   kweli, utukufu wa Bwana ni **mkubwa**.

4. Mkono wako wa kuume unanisali**misha**,
   Bwana atatimiliza kwangu aliyonite**ndea**.
   Ee Bwana, wema wako ndio wa mi**le**le,
   usiache kazi ya mikono **yako**.

amanijeannot@gmail.com